

**Jibu:** Tusome,

“**Ganjo**” ni mahali palipoharibika.. Jengo lililoharibika linaitwa “**Ganjo**” yakiwa mengi yanaitwa “**maganjo**”, mji ulioharibiwa aidha kwa vita au kwa janga fulani pia unaitwa “**Ganjo**”.

**Katika biblia neno hili limeonekana mara kadhaa..**

*Walawi 26:30 “Nami nitapaharibu mahali penu palipoinuka, na kuziangusha sanamu zenu za jua, nami nitaitupa mizoga yenu juu ya mizoga ya sanamu zenu; na roho yangu itawachukia.*

*31 Nami nitaifanya MIJI YENU IWE MAGANJO, na mahali penu patakatifu nitapatia ukiwa; wala sitasikia harufu ya manukato yenu yapendezayo.*

*32 Nami nitaitia hiyo nchi ukiwa; na adui zenu watakaokaa huko wataistaajabia”*

**Tusome pia...**

*Ezekieli 29:12 “Nami nitaifanya nchi ya Misri kuwa ukiwa, kati ya nchi zilizo ukiwa, na miji yake, kati ya miji iliyoharibika, ITAKUWA MAGANJO muda wa miaka arobaini; nami nitawatawanya Wamisri kati ya mataifa, nami nitawatapanya kati ya nchi mbalimbali.”*

Neno hili pia unaweza kulisoma katika mistari ifuatayo likiwa na maana hiyo hiyo..**Walawi 26:33, 2Nyakati 34:6, Ayubu 3:14, Isaya 6:11, 7:19, Yeria 4:7, Ezekieli 6:14, 36:38, na Amosi 9:14.**

Vile vile hii dunia siku moja itafanyika kuwa “**GANJO**”, kutokana na dhambi!.. Bwana ataiharibu kwa moto kama alivyoiharibu nyakati za Nuhu, kwa maji.

*2Petro 3:6 “kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.*

*7 Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu”.*

Je umeokoka? Kama bado, saa ya wokovu ni sasa, tupo mwisho wa nyakati.

Maran atha.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

### **Mada Nyinginezo:**

**Agano ni nini? na kuna aina ngapi za maagano?**

**Miji ya Tiro na Sidoni ni miji gani kwasasa?**

**Kama Malkia Esta alijipamba je! Kuna ubaya gani wanawake wa wakikristo wa leo kujipamba?.**

**TAA YA MWILI NI JICHO,**

## VICHEKESHO NA UTANI MADHABAHUNI

### Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp

[Print this post](#)